## Maswali

1. Nani alikuwa akisaidia Musa alipoenda kuzungumzia Farao?
2. Musa aliambia Farao ujumbe gani kutoka kwa Mungu?
3. Musa alisema eti nini itafanyika ikiwa Farao hatawaachilia Waisraeli waende?
4. Nini ilifanyika Haruni aliponyorosha fimbo yake juu ya Mto wa Nile?
5. Nini ilitoka kwa maji Farao alipokataa kuachilia watu waende?
6. Tauni gani ilitokea baada ya vyura?
7. Tauni gani ilitokea baada ya chawa?
8. Tauni nne zilizofwata zilikuwa gani?
9. Baada ya kila tauni, Farao alisema atafanya nini?
10. Farao alifanya nini Mungu alipoondoa tauni?

## Majibu

1. Mungu alikuwa akisaidia Musa.
2. Waruhusu Waisraeli waondoke Misri.
3. Mungu atatuma tauni kwa nchi ya Misri ikiwa Farao hatatii Mungu.
4. Maji ya Mto wa Nile yaligeuka na kuwa damu.
5. Maelfu ya vyura yalitoka kwenye mto.
6. Baada ya tauni ya vyura kulitokea tauni ya chawa.
7. Baada ya tauni ya chawa kulitokea tauni ya inzi.
8. Kulikuwa na ng’ombe kukufa, mvua ya mawe, nzige na giza.
9. Farao alisema atawaruhusu Waisraeli waende.
10. Farao alibadilisha mawazo yake na hakukubali Waisraeli waende.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 1    Mwaka wa 3

# 14 Tauni huko Misri

## Marejeo

Kutoka 7:19 – 21;  8:1 – 5 na 16 – 17 na 20 – 24;
9:1 – 4 na 8 – 10 na 22 – 24;  10:12 – 15 na 21 – 23

## Kiini cha somo

Kuonyesha nguvu za Mungu za ajabu zilizofanya Farao aachilie Waisraeli watoke Misri.

## Maneno maalum

14.1 Farao + Musa + Mungu + wacha watu wangu waende + tauni + Waisraeli wasiende

14.2 Mto wa Nile + maji + damu

14.3 Siku 7 + Farao + Waisraeli wasiende + vyura

14.4 Tauni ya chawa + Farao + achilia watu waende + hakuna chawa + badilisha mawazo + inzi + badilisha mawazo

14.5 Ng’ombe + mvua ya mawe + nzige + giza + Farao + badilisha mawazo kila wakati

**14.1** Farao alikuwa mfalme waajabu na wa nguvu. Alikuwa na mamlaka yote juu ya Misri. Kila kitu alichoamrisha, kilifanywa mara moja. Yeyote aliyemkasirisha lazima aliuawa.

Musa alikuwa mchungaji kwa miaka arobaini. Hakukuwa na uwezo au mamlaka juu ya nchi ya Misri. Lakini Mungu alimwambia aende kwa Farao mkuu wa nchi ya Misri na awaruhusu Waisraeli watumwa wake waondoke Misri. Farao hakufahamu chochote juu ya Mungu wa kweli. Hakutaka kuwapoteza watumwa wake waliomfanyia kazi ya kujenga.

Musa aliogopa sana alipokuwa akienda kumuona Farao. Lakini Mungu alikuwa amemwahidi kumsaidia. Musa alimwambia Farao, "Bwana Mungu wa Israeli asema hivi, 'Waruhusu watu wangu waende."' Farao alijibu kulingana na matarajio ya Musa, "Bwana ni nani ndiyo ni mtii na niwaruhusu Waisraeli waende. Sijui huyo Bwana na sitawaruhusu Waisraeli waende."

Musa na Haruni waliambia Farao kwamba asipowaruhusu Waisraeli waende, Mungu atatuma tauni kwa nchi ya Misri. Lakini Farao alikasirika sana na hakuwasikiliza. Alifanya kazi ya Waisraeli watumwa wake kuwa mzito zaidi. Mungu alimwambia Musa kwamba atafanya Farao awaruhusu Waisraeli waende. Mungu atateza Farao kwa kutuma tauni kwa nchi ya Misri.

**14.2** Kulikuwa na mto mkubwa Misri ulioitwa Mto wa Nile. Siku iliyofuata Musa na Haruni walikutana na Farao akiteremka kwa Mto wa Nile kwenda kuoga. Walimwambia akikataa kuwaruhusu Waisraeli waende, Mungu atageuza maji ya nchi yote iwe damu. Farao alipokataa, Haruni alinyosha fimbo yake juu ya Mto wa Nile na maji yote yaligeuka yakawa damu. Hakuna mtu yeyote angeweza kuoga hayo maji nyekundu ya ulimbo, kwa hivyo watu walikuwa na kiu.

**14.3** Baada ya siku saba, Musa alienda kuona Farao tena. Aliambia Farao kwamba asipowaruhusu Waisraeli watoke Misri, Mungu atajaza nchi ya kwa vyura. Lakini Farao alikataa kuwaruhusu. Haruni alinyosha fimbo yao juu ya mto na maelfu na maelfu ya vyura waliruka nje. Kulikuwa na vyura ndani ya vitanda, chini ya miguu kila mahali hata kwa vyombo vya kupikia.

Farao hakufurahia kuwa na vyura kila mahali. Bunde tu aliita Musa na kumwambia kwamba Mungu akiondoa vyura, atawaruhusu Waisraeli waende. Siku iliyofwata Mungu aliondoa vyura. Lakini bunde tu vyura walipoondolewa Farao alibadilisha mawazo na hakuruhusu Waisraeli waoondoke.

**14.4** Musa na Haruni walimwambia Farao kwamba Mungu ataleta tauni ya chawa lakini Farao hakusikiliza. Mungu alileta chawa na kila mtu alifunikwa na chawa. Farao aliita Musa tena, akamwambia kwamba atawaruhusu Waisraeli waondoke ikiwa Mungu atatoa chawa. Lakini baada ya Mungu kuondoa chawa, Farao alibadilisha mawazo na hakuwaruhusu Waisraeli waondoke.



Baadaye kulikua na inzi kwa nchi yote ya Misri, lakini baada ya Mungu kuwaondoa, Farao alibadilisha mawazo tena na hakuwaruhusu Waisraeli waondoke.



**14.5** Mungu alituma tauni zingine tano kwa nchi ya Misri. Alituma tauni iliyoua ng'ombe, tauni ya majibu kwa watu Wamisri wote na tauni ya mvua ya mawe iliyoua wanyama na kuharibu mimea zote. Halafu akaleta tauni ya nzige waliokula majani mabichi yote kwa nchi ya Misri. Tena Mungu alileta tauni ya giza totoro yenye mtu hangeona chochote kwa siku tatu. Kila tauni iliyokuja Farao aliambia Musa kwamba atawaruhusu Waisraeli waondoka. Lakini unajua nini! Mungu alipoondoa tauni tu, Farao alibadilisha mawazo yake na hakuwaruhusu Waisraeli waende.

Lazima Musa alijiuliza kwamba ni lini Farao atabadilisha mawazo yake! Kwa somo lijalo tutajifunza vile Mungu alileta tauni ya kumi na ya mwisho na vile Waisraeli waliondoka Misri na kusafiri kwenda nchi yenye Mungu aliwaahidi.